**MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA 17 WA URA SACCOS ULIOFANYIKA TAREHE 28-11-2025 JIJINI ARUSHA**

1. Kwa kuwa chama kimekuwa kikipitia changamoto ya Ukwasi, ili kukabiliana na Changamoto hii, mkutano mkuu umeazimia kuongeza kiwango cha Akiba ya lazima kutoka:
   - Shilingi 30,000/= hadi kufikia Tsh 50,000/= kwa mwanachama wa kawaida.
   - Shilingi 150,000/= kwa menejimenti makao makuu na matawi.
   - Shilingi 100,000/= kwa wawakilishi na
   - Shilingi 200,000/= kwa wajumbe wa bodi na kamati ya usimamizi.
2. Ili kuhamasisha uwekaji wa Akiba na Amana, mkutano mkuu umeazimia kuongeza kiwango cha Riba juu ya Akiba na Amana kama ifuatavyo;
   - Akiba kutoka 5% hadi 8%.
   - Amana kutoka 5% hadi 9%.
3. Kwa kuwa elimu ya kikanda kwa wawakilishi imeendelea kuwa yenye mafanikio na kuleta tija katika chama, mkutano mkuu umeazimia elimu kwa wawakilishi iendelee kutolewa kuanzia mwezi februari hadi mwezi machi 2026 ili kupata uelewa wa Pamoja itakayosaidia wawakilishi Kwenda kutoa elimu iliyo sawa kwa wanachama.
4. Ili kuongeza Motisha ya kuhudhuria vikao vya kutoa elimu kwa wanachama, mkutano mkuu umeazimia,kiwango cha Posho ya kikao kiongezeke kutoka 60,000/= hadi Tsh 70,000/= na kiwango hiki kitagawanjwa katika akaunti za wanachama kwa mgawanyo ufuatao;
   - Hisa Kiasi cha Tsh 50,000/=
   - Amana kiasi cha Tsh 20,000/=
5. Ili kuimarisha mtaji wa chama,Mkutano mkuu umeazimia:-
   - Kuhamisha kiasi cha Shilingi Bilioni moja (Tsh 1,000,000,000/=) kutoka katika mfuko wa kinga ya ndani ya Mikopo Kwenda kwenye limbikizo la ziada.
   - Gawio (Dividend) kwa wanachama liwekwe katika akaunti ya Hisa ya kila mwanachama kulingana na kiwango stahiki atakachokipata.
6. Ili kuendeleza lengo la ujenzi wa jengo la ofisi ya chama, mkutano mkuu umeazimia kutumika Tsh 1,000,000,000/= kutoka katika mfuko wa kinga wa ndani na maendeleo kwa awamu ya pili.

7. Kutokana na kukamilika kwa mfumo wa maombi ya mkopo kwa watumishi wa umma kidigitali kupitia mfumo wa ESS, mkutano mkuu umeazimia kuanzia januari 2026, mkopo wa uwiano wa mshahara uanze kutolewa kwa kupitia mfumo huo.